

Cheche za Fikra

JUZUU 6 TOLEO 23

JANUARY 20, 2009

KIJARIDA CHA BURE— UKISHASOMA MPE MWINGINE—USIBANIE!

MAKALA MAALUM

MAJIBU KWA RAIS ATCL ILIFIKA HAPA HIVI USHAHIDI WOTE WAFUNULIWA

**Na. Fred
Katunzi**


Kama mi-pango iliyopo sasa itatekelezwa kama inavyokusudiwa, basi ndege za Shirika la Ndege la Tanzania zitakuwa angani kuanzia tarehe 23 mwezi huu katika kuitikia wito wa Rais Kikwete wa ndege hizo kurudi angani mapema inavyowezekana.

Tumeguswa kwa namna ya pekee na mshangao wa Rais aliutoa mwishoni mwa juma alipokutana na uongozi wa Wizara ya Miundombinu na wale wa Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) Ikulu katika kile kinachoelezwa kuwa ni mzunguko mwingine wa Rais kutana na viongozi wa



wizara mbalimbali. Kilichotugusa zaidi ni kauli ya Rais iliyonukuliwa na vyombo mbalimbali vya habari akionyesha mshangao wa jinsi gani

kampuni ya ATCL imefika hapa ilipofika hadi kusimamisha usafiri wa ndege zake.

(Inaendelea Uk. 2)


Benjamin. G. Mwalukasa
Mhariri

Kijarida Ulichoshika

- Kinatoka kila Jumanne
- Ni cha bure kabisa!
- Kisichofungamana na chama chochote au fisadi yeyote!
- Kiko huru, kinathubutu, na hakiogopi mtu au hoja yoyote.
- Ni kijarida chako!
- Haki zote za kuchapa na kunakili zimeruhusiwa!

Ndani ya Toleo Hili

ATCL ilifikaje hapa?	1
Hoja ya Mwanakijiji	1,4
ATCL ilifikaje hapa?	2,3,4
Hoja ya Mwanakijiji	4
Kukatika Umeme	5
Da' Jessie: Mifupa hii!	5
Picha, Katuni na Maoni	6

HOJA YA MWANAKIJJI — ASANTE BUSH; KARIBU OBAMA

Leo dunia inashuhudia kile ambacho hakikutarajiwa kutokea miaka ya karibuni. Taifa lenye nguvu zaidi duniani lina muapisha mmoja wa watoto wake mwenye asili ya Africa Bara maskini zaidi duniani kuwa Rais wake wa 44.

Kwetu sisi Watanzania hata hivyo hatuna budi kujiuliza

kuapishwa kwa Obama kuwa Rais wa 44 wa Marekani kuna maana gani kwetu kama Taifa.

Kuweza kufikia jibu hilo hatuna budi kukiri kuwa hadi hivi sasa hakuna Rais wa Marekani aliyegusa maisha ya Watanzania wengi zaidi kama Rais George W. Bush anaye-



maliza muda wake leo saa 5:59 za asubuhi. **(Inaendelea Uk. 4)**

KILICHOIFIKISHA ATCL HAPA NI HIKI

Rais Kikwete alinukuliwa kutoa kauli hizi ambazo tunaamini zinahitaji kujibiwa kwa ukweli na uwazi wote. Aliuliza kama kuhitaji majibu “Je ni msaada gani na kiasi gani cha fedha mnahitaji kuweza kuanza tena kutoa huduma?” na pia “Nataka kujua kiini cha matatizo yetu ya karibuni mpaka tukasimamisha kurusha ndege zetu? Tulifikaje hapo?” lakini kubwa zaidi ni hili hapa “Je tume-



toka na kama tumetoka, tunafanya nini ili tusirudi kwenye matatizo hayo?”

Tunakusudia kujibu maswali yote hayo lakini tukianza na hilo la mwisho. Tunaamini hatua zinazochukuliwa sasa hasa uamuzi wa kutoa fedha nyingi zaidi kwa ATCL ilivyo sasa hakusaidi kutatua matatizo yaliyopo na kwa hakika hakuhakikishi kuwa shirika halitarudi kwenye matatizo hayo. Tunaamini kinachofanywa ni kujaribu kuondokana na soni na aibu ya shirika kusimamisha huduma zake na hivyo kujarib kuharakisha kuweka ndege zetu hewani.

Mababu walisema “haraka haraka haina baraka”. Tunaamini jitihada za kuharakisha kurudisha ndege zetu hewani katika mazingira na chini ya uongozi uliopo kwa hakika ni maandalizi ya gharama kubwa ya kuilipa kama Taifa aidha kwa mali au kwa damu. Jitihada zozote zile za kuiokoa ATCL tunaamini ni lazima ziwe za kisayansi, zilizotafakariwa kisomi, na ambazo zinaongozwa na timu yenye rekodi na uwezo wa kutuonesha njia katika giza hili totoro. Nje ya hapo, jitihada hizi zinafanywa ili kumridhisha Rais.

Kwa hiyo hilo swali la mwisho jibu lake ni jepesi; tusifanye haraka au papara ya kurusha ndege zetu ilimradi na sisi tuwe na mbawa zetu zikipasua anga la Afrika na bendera yetu kupepereshwa mawingu.

Tutatumia muda kidogo kujibu swali la pili ambalo linauliza kuhusu “kiini cha matatizo” ya ATCL. Yote tunayoyaandika kwenye kijarida chako hiki unaweza kuyapata kama ushahidi kwenye tovuti yetu ya mwanakijiji.com.

Hotuba ya Bajeti 2007/2008

Aliyekuwa Waziri wa Miundo Mbinu katika miezi ya kwanza ya utawala wa Rais Kikwete Mhe. Andrew Chenge alihutubia Bunge mwaka 2007/2008 katika ile hotuba ya bajeti ambayo ilitarajiwa kuelezea mipango mbalimbali ya Wizara yake. Alipozungumzia kuhusu ATCL Mhe. Chenge alilitaarifu Bunge kuwa ushirika kati ya ATCL na Shirika la Ndege la Afrika ya Kusini (SAA) umefikia kikomo. Bw. Chenge alitangaza na kusema kuwa “Napenda kutoa taarifa kuwa SAA ilikubali ombi la Serikali ya Tanzania la kujitoa katika ubia wa ATCL. Makubaliano ya kusitisha ubia huo yalisainiwa Johannesburg, Afrika ya Kusini Agosti, 2006, ambapo Serikali ya Tanzania ilinunua hisa zilizokuwa za SAA ndani ya ATCL zipatazo asilimia 49 na hivyo kumiliki kampuni hii kwa asilimia mia moja.” Bw. Chenge akatangaza kama ahadi kuwa “Hivi sasa Serikali inaweka mikakati ya kuiimarisha ATCL ili iweze kufikia lengo la kuwa na Shirika la Ndege la Taifa lililo imara.”

Kwa hiyo kiini cha kwanza na cha pekee kilichozaa matatizo ya ATCL ni kuwa serikali haikusimamia ahadi yake kwa Taifa ya “kuiimarisha ATCL” ili hatima kuwa shirika la ndege ambalo ni “Imara”. Hivyo basi, kukosekana kwa usimamizi wa makusudi (kama tutakavyoonesha) kwa mmiliki wa shirika hilo (ATCL) ndiko kulikofungulia bwawa la uzembe ambalo lilifurika kuto-kuwajibika, ufujaji, na ubadhirifu.

Kutokana na hilo la serikali yaliyofuatia yalikuwa ni matokeo tu ya hilo la serikali kutokuonesha usimamizi. Ni yapi hayo basi.

1. Uteuzi wa bodi na uongozi wa juu wa ATCL.

Katika hotuba yake ile ya bajeti Waziri Chenge alitangaza kuwa mojawapo ya mipango ya serikali kutimiza ahadi yake hiyo kwa Taifa ni pamoja na “uteuzi wa Bodi na Uongozi mpya wa ATCL”. Kati ya watu ambao hawakutarajiwa kuliongoza shirika hili kuelekea Uimara ni timu ya Balizi Mustafa Nyang’anyi (Bodi) na David Mattaka (Utendaji). Mwanzoni kabisa tuliyaona matatizo ya timu hii mwaka huo huo katika lile lililokuja kujulikana kama

sakata la mahujaji ambapo maelfu ya Waumini wa dini ya Kiislamu walijikuta wakihaha na kuhangaika baada ya ATCL kushindwa kuwasafirisha ndani ya muda kuelekea kwenye Hija huko Saudia.

Jambo lile kama lingekuwa limetokea nchi nyingine lingeweza kabisa kumfukuzisha mtu yeyote kazi lakini katika nchi yetu na chini Chenge hakukuwa na hatua zozote zilizochukuliwa zaidi ya kufanya mipango ya haraka haraka na kuhidi kuwa jambo hilo halitokea tena. Kwanini waliendelea na majukumu yao. Hatuna majibu kwa sasa.

2. Ukodishaji wa dege la Airbus A320-214 kutoka Wallis Trading ya Liberia.

Tulikuwa chombo cha kwanza kulifunua suala hili na kuwaangaliza serikali kuhusu mkataba huo (unaweza kuusoma kwenye mwanakijiji.com). Tunaamini kwa asilimia 100 kuwa uamuzi wa ukodishaji wa dege hilo kubwa kwa masharti yaliyokuwepo na mchakatoo mzima hadi kuweza kuli-leta nchini ulikuwa ni uamuzi usio na maono, uliofungua mlango wa ufisadi, na kuwa chanzo cha ufujaji mkubwa kabisa wa fedha za walipa kodi wa Tanzania.

Ukodishaji wa dege hilo kubwa ulifanywa baada ya ATCL kuamua kubadilisha ndege zake hasa za Boeing na kutafuta ndege nyingine. Vyanzo vya kuaminika vimeambia “Cheche” kuwa tayari serikali ina mkataba wa ununuzi wa madege mapya ya Airbus (319/330) yanayotarajiwa kuingia nchini mwaka 2012. Kwa mujibu wa chanzo hicho kutokana na kukosekana kwa ndege mpya toka Airbus ATCL iliamua kukodi toka Wallis Trading kwa ushauri wa Airbus.

Mkataba wa ukodishaji wa dege hilo ulio-



KARIBU MWANAKIJIJI.COM

saniwa tarehe 9 Oktoba, 2007 unaone-sha kuwa mkataba huo ulikuwa ni wa kiasi cha dola milioni 30 kwa miaka mitano au "such other amount as Lessor may require from time to time provided such other amount does not exceed 120% of the fair market value of the Aircraft." Ni kwanini tunaingia mkataba wenye kutokutabirika kwa gharama kama huko. Unaposema kuwa "such other amount as lessor may require from time to time" una maana gani? Tutawaacha wanasheria wafafanue kipengele (clause) kama hicho na kinaavyoweza kutafsiriwa.

Mkataba huo unaelezea malipo ya kila mwenzi ambayo ATCL ilitakiwa kulipa Wallis Trading. Kwa mujibu wa ibara ya 5.3(c) ya mkataba huo shirika la ATCL linatakiwa kulipa kampuni hiyo dola 370,000 kila mwezi katika kuhudumia deni lake la kuikodi ndege hiyo. Zaidi ya kiasi hicho ATCL inatakiwa kulipia dola nyingine 28,500 kila mwezi kulipia gharama nyingine mbalimbali kama "supplemental rent" (kodi ya ziada) ya matengenezo ya vitu mbalimbali vya ndege hiyo. Zipo na gharama nyingine zinazotegemea masaa ya ndege angani.

Kwa hiyo kwa mwezi tu ATCL (tena kwa ndege moja ilitakiwa kulipa dola karibu 400,000 (karibu milioni 450Tsh).

Hilo lingekuwa na unafuu endapo dege hilo lingefika nchini kabla ya Disemba 2007 kama ilivyopangwa na kuanza safari mara moja. Badala yake ndege hiyo imefika karibu mwezi wa tano 2008 na muda wote huo ATCL ilikuwa tayari imeanza kuhudumia deni lake hilo bila ya ndege kuwa angani!. Kwa maneno mengine serikali ilikaa pembeni kuangalia ATCL ikilipa deni la kitu isichotumia!.

Hilo lilisababishwa na serikali kuttoa udhamini wake kwa ATCL kama Mkataba unavyosema (Guarantor: The Government of Tanzania). Kwa mujibu wa Mkataba huo serikali ilitakiwa itoe barua ya udhamini wa ukopaji huo wa ATCL usiopungua kiasi cha dola milioni 10. Udhamini huo ulitakiwa (kwa mujibu wa ibara ya 5:15(a)) kutolewa ndani ya siku tatu baada ya kutiwa sahihi na si zaidi ya tarehe 10 Oktoba, 2007.

Mkataba huo unasema wazi kuwa kuchelewesha kutolewa kwa udhamini huo kutaambatana na adhabu ya dola elfu sitini (60,000) kwa kila mwezi ambapo udhamini huo hautatolewa. Serikali haikutoa udhamini huo hadi mwezi

wa nne 2008 (unaweza kusoma barua hiyo kwenye mwanakijiji.com).

Hivyo kwa haraka haraka tunaweza kusema tangu mwezi wa kumi hadi mwezi wa nne ambapo udhamini ulitolewa imepita miezi sita pasipo udhamini huo. Hivyo miezi hiyo yote ATCL ilitakiwa kulipa adhabu ya dola 360,000 pamoja na gharama ya kodi ambayo ni dola 498,000 kwa mwezi ATCL katika miezi sita hiyo ya mwanzo wa mkataba tayari ilikuwa na deni la dola 3,348,000/ (matumizi bila kuzalisha).

Hii ina maana ya kwamba, vyovyote vile itakavyokuwa ndege ya Airbus 320 ilitakiwa kuanza kulipa deni hilo mara moja na kwa haraka. Wakati huo huo, serikali ilikuwa imeanza mazungumzo na makubaliano na kampuni ya Airbus ya Ujerumani kuweza kununua dege jingine jipya na uwezekano wa kununua nyingine mika michacha baadaye.

Cha kushangaza hata hivyo katika hotuba yake Bungeni Mhe. Chenge hakueleza mpango wowote wa kukodi Airbus mwaka 2007. Zaidi ya yote hatukumbuki wakati wowote ambapo mchakato wa kutangaza ukodishaji wa ndege ilitangazwa katika vyombo vyetu au kwa Watanzania na kama sheria ya Manunuzi ya Umma ilifuatwa au la. Ni Kamati Teule ya Bunge au Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma inaweza kutuonesha hilo.

Sasa hapa tunaona matokeo ya serikali kutokuwa mwangalifu kwa shirika hili kiasi kwamba katika jitihada za kujinasua li-naanza kwa kutengeneza deni kubwa la bilioni karibu mbili na nusu.

Gharama nyingine kutokana na ukodishaji Airbus

Wakati ATCL inakodisha dege hilo la Airbus tuliweka hadharani taarifa kwamba ndege hiyo waliikuta ikiwa na uchakavu wa ndani ambao uliwashangaza hata wamhandisi wake waliobobea. Taarifa yetu hiyo ilitumia msingi wa Taarifa ya kampuni ya AirClaims iliyokodishwa na waten-genezaji Airbus kuifanyia ukaguzi ndege hiyo na kutoa taarifa kwao pamoja na taarifa ya ukuaguzi iliyofanywa na wao wenyewe ATCL mara baada ya kufika El Salvador na kuikagua A320. Jaribio la kutaka Wallis Trading igharimie matengenezo hayo liligonga mwamba na matokeo yake ATCL ikabidi ilipie matengenezo ya vitu zaidi ya 100 ili kuifanya ndege hiyo iwe tayari kwa safari.

Katika kufanya hivyo ATCL iliingia



Dash 8 ya ATCL

mkataba mwingine na Aeroman wa kufanyia matengenezo ndege hiyo katika gereji yake huko El Salvador. Mkataba huo awali ulikisiwa kuwa wa karibu dola laki 95,000 hivi. Hata hivyo katika ankra kutoka Aeroman kwenda ATCL ya tarehe 18 Machi, 2008 gharamaya matengenezo hayo ilikuwa inafikia dola 270,188.

Hii ina maana ya kwamba, wakati tayari ATCL ilikuwa na deni la milioni 2.3 tayari pia lilikuwa na deni la dola 270,000 kutoka Aeroman. Serikali ilikuwa inajua juu ya hili au ilikuwa haijui (matokeo ya yote hayo mawili ni ya kutisha).

Gharama nyingine ambazo zinafikia dola laki moja kwa Mhandisi wa ATCL aliye-kuwa El Salvador akiifuatilia na kuisubiria ndege hiyo hadi ilipoletwa nchini (vyanzo mbalimbali vinatadokeza kuwa alikuwa analipwa dola 400 kwa siku!). Na ndege hiyo ilipoletwa nchini hatukuwa na marubani wala wataalamu wa kuifanyia matengenezo. Hivyo tukaingia mkataba na kampuni nyingine kuleta marubani na kampuni nyingine (toka Mauritius) kutusaidia katika masuala ya matengenezo.

Ununuzi wa Dash 8-300

Wakati ATCL inahangaika na deni la Airbus (Wallis Trading) shirika hilo likaa-mua kuingia mikataba miwili ya kununua ndogo nyinginei kwa gharama ya dola milioni 8 kila moja (dola milioni 16 kwa jumla). Hili nalo tunalidokeza tu hapa kuonesha kuwa ahadi ya serikali kuwa ilitaka kuifanya ATCL kuwa imara ilikuwa ni ahadi isiyotekelezeka tukiangalia mwanga wa "mpango wa biashara" uliotangazwa na Chenge kuwa unaandaliwa.

**Soma
bure**



Enzi za Fahari yake— Air Tanzania Boeing 767

Waziri Kawambwa akilihutubia Bunge alielezea mipango mingine ya kuongeza ndege kama ifuatavyo "Kampuni ina jumla ya ndege 6, 3 za kukodi na 3 za Kampuni yenyewe.... Mikakati mingine ni kununua ndege mbili zenye uwezo wa kuchukua abiria 72 kila moja.. Kampuni inatarajia kukodi ndege nyingine ya B737-200 au ndege nyingine yenye ukubwa huo.."

Sisi tunajiuliza, kampuni ATCL ina matatizo ya fedha kama kina Nyang'anyi walivyoweza kuishawishi serikali inaweza vipi kupanga miradi mikubwa ya matumizi makubwa ya fedha namna hii bila ya kuwa na uhakika mzuri wa mapato?

Hayo ni machache tu ambayo tumejaribu kuyadokeza. Na hapo hatujaweka gharama za nguvu kazi, vitendea kazi vingine n.k. Kilichotushtua zaidi ni kuwa

wakati shirika liko katika mpango wa Uimara viongozi wake kadhaa waliachwa na serikali kuingia mikataba ya ununuzi wa magari ya kifahari kwa matumizi yao. Na ni viongozi hao hao ambao leo w mediriki kuishawishi serikali (nayo ikashawishika) kuwa tatizo la ATCL ni fedha!

Tunasikitika kwamba Rais Kikwete na serikali yake wamepewa taarifa juu ya matatizo ya ATCL kwa mwa mzima sasa. Tunasikitika kwamba badala ya kuchukua hatua hasa za kulinasua shirika hilo serikali imeendelea kukaa chini na kufanya "mazungumzo". Tunasikitika kwamba kuna imani kuwa uongozi uliopo ndiyo upewe jukumu ya kulinasua shirika hilo. Kwamba, uongozi uliopanga na kutekeleza mipango ya kushangaza ndio hao hao wamekinga mikono tena kuomba fedha zaidi. Msimamo wetu mara hii na ya mwisho ni kuwa; tatizo la ATCL siyo fedha bali

uongozi wenye maono, uongozi wenye kuweka maslahi ya Taifa mbele na kwa hakika uongozi ambao unaweza kweli kuwajibika na fedha za walipa kodi wa Tanzania. Kwa jinsi serikali ilivyosimamia ATCL tangu mkataba wao na SAA uvunje inaonekana ni kama waliachwa wajifanyie mambo wenyewe.

Tunaamini (kwa ushahidi wote uliopo na tunaouweka kwenye tovuti yetu kwa watu kuamua wenyewe) Mbaguzi Mkuu wa serikali alitakiwa awe amepitia mahesabu yote ya ATCL mara moja na kwa kushtukiza; ilitakikana uongozi uliopo hapo sasa ungesimamishwa kazi mara moja hasa baada ya tuhuma nzito kuwa Mwenyekiti wa Bodi hiyo aliilazimisha ATCL kuingia kwenye biashara ya kubeba mahujaji wakati shirika halikuwa na uwezo huo. Uongozi huo ni pamoja na bodi nzim ya ATCL na na watendaji wote wa juu wakiongozwa na Bw. David Mattaka.

Tunaamini kuwa tatizo la ATCL liko mikononi mwa serikali ya Watanzania. Serikali hii ndiyo imelivurunda shirika hili na ni wao wenyewe walitengeneza. Hakuna sababu ya kukimbilia Uchina au Afrika ya Kusini. Aidha tutumie uwezo na nguvu zetu kuliokoa kitalaamu au tuliache life kabla halijau!

Tukiongozwa na dhamira safi, tumefanya kila tuliloweza kuliamsha Taifa kuhusu ATCL kama tulivyofanya kuhusu Richmond, Ukraine, vifo vya watoto Tabora n.k. Hatutaandika tena ripoti yeyote kuhusu sakata hili kwani tuliyoyaandika kwa mwaka mzima, yanatosha. Mpira sasa uko kwao. Sisi yetu macho na masikio.

HOJA YA MWANAKIJIJI: ASANTE BUSH, KARIBU OBAMA

Kwa wengine Rais Bush anapimwa kutokana na sera zake huko Iraq, Sudani, Afghanistan au hata msimamo wake wa kuinga mkono Israeli katika mgogoro wa Palestina. Kwetu sisi Watanzania hata hivyo tutakuwa hatutendi haki endapo tutamhukumu Bush kwa vipimo vya mahusiano yake na nchi nyingine au jamii nyingine ya watu.

Bush kama vile Obama anavyokuja tutampima kutokana na sera zake kwa Tanzania na urafiki wake kwa watu wetu. Rais Bush kwa kipimo chochote kile alikuwa ni rafiki kwa Tanzania. Chini ya uongozi wake watu wetu wamepata nafasi ya kuishi tena kutokana na sera yake ya kupambana na Ukimwi na maambukizo ya VVU.

Chini ya uongozi wake miradi mbalimbali ya maendeleo imetokelezwa Tanzania (kuanzia ujanzi wa maabara ya kisasa Muhimbili) na ujenzi wa vituo mbalimbali vya afya Tanzania bara na Zanzibar.



Hakuna ubishi wowote ule kuwa msaada wa Marekani katika masuala mbalimbali na hasa uwakilishi wa Balozi

Mark Green umefungua ukurasa mpya wa ushirikiano kati ya nchi zetu mbili.

Ninafahamu serikali imetuma ujumbe wa watu kutuwakilisha kwenye kuapishwa

kwa Rais Mteule Obama. Ni matumaini yangu kuwa Rais Obama atakapomaliza muda wake tutaweza kusema kama alivyosema Rais Kikwete kuhusu Bush kuwa alikuwa ni rafiki kwa Tanzania.

Kipimo pekee ambacho tunapaswa kumpima nacho Obama siyo rangi yake, siyo ahadi zake, au maneno yake ya matumaini bali ni jinsi gani Tanzania na Afrika kwa ujumla itaonekana kwenye sera za Marekani. Karibu Obama, Asante na Kwaheri Bush.



CHECHE PEKEE

KUKATIKA UMEME NI KHITILAFU—NGELEJA

Na. Mahmoud Rashid

Waziri wa Nishati na Madini Mhe. William Ngeleja amesema kuwa tatizo la kukatika umeme lililotokea sehemu kubwa ya nchi jana usiku lilitokana na khitilafu ambazo zilifanyiwa uchunguzi mara moja na kutatuliwa.

Akizungumza na kijarida hiki jana jioni muda mfupi baada ya umeme kuanza kurejea sehemu mbalimbali nchini Bw. Ngeleja alisema kuwa ingawa alikuwa nje ya Dar taarifa za awali alizozipata zinaonesha kuwa kulikuwa na khitilafu ambayo hakuweza kuifafanua mara moja.

Cheche ilijaribu kumpata Naibu Waziri wa Nishati na Madini Mhe. Adam Malima ambaye naye alikuwa katika harakati za kutafuta ufumbuzi na taarifa zaidi kuhusu kukatika huko kwa umeme ambako kuliwashtua wananchi wengi.

Bw. Malima alisema kuwa yeye naye kama wananchi wengine walikutwa na kukatika kwa umeme pasipo taarifa yoyote ya awali na aliahidi kutoa taarifa zaidi pindi chanzo cha tatizo hilo kitakapokujulikana kwa upana wake.

Jana Jumatatu majira ya saa 12 za jioni

umeme ulikatika karibu nchi nzima katika hali ambayo ilishtua watu wengi kwani siyo tu siyo jambo la kawaida lakini kutokana na mfumo wa ugavi wa umeme uwezekano wa nchi nzima kukosa umeme wa gridi ya Taifa ni mdogo sana.



Bw. W. Ngeleja

Mwananchi mmoja aliyetuma ujumbe kwa mhariri kutoa taarifa hizo za kukatika umeme alisema kuwa haelewi inawezekana vipi mikoa mbalimbali ambayo ina vyanzo mbalimbali vya umeme yote kukosa umeme kwa wakati mmoja.

Hata hivyo hadi tunakwenda mitamboni haijajulikana kama ni kweli mikoa yote ilikosa umeme au baadhi yake huku kukiwa na uhakika kuwa Jiji la Dar lilikosa umeme kwa muda wa karibu masaa mawili.

Hata hivyo baadhi ya wadadisi wa mambo ya nishati wameanza kuwa na shaka kuwa tukio la kukatika umeme limekuja karibu wiki moja kamili tangu mtikisiko mwingine

kwa jiji la Dar kutokea pale vituo vya mafuta viliposhindwa kutoa huduma hiyo kwa madai kuwa "hakukuwa na mafuta".

Madai hayo yaliishangaza jamii kwani wiki chache kabla Naibu Waziri Malima alilihakikishia Taifa kuwa mafuta yapo. Kukosekana kwa umeme siku chache baada ya kukosekana kwa mafuta ambayo ni chanzo cha nishati kumetafsiriwa kwa namna tofauti.

"Unajua bado watu wa Dowans wanataka kutuuzia mitambo, na hakuna kitu kizuri cha kutulazimisha kama kukosa umeme" alidai msomaji wetu aliyeko Tanga. Msomaji huyo Bw. Ramadhani (jina la pili tumelishikilia) amedai kuwa "yaweze kana bado kuna juhudi ya kuhakikisha kuwa tunaona ipo haja ya lazima ya kununua mitambo ya Dowans ili kupata nishati ya umeme kwani 'wale' jamaa bado hawajakubali kuwa wamenyang'anywa keki mdomoni".

Hata hivyo, vyanzo vyetu vya kuaminika vimesema kuwa baadaye leo taarifa itatolewa na uongozi wa TanESCO kuelezea chanzo cha tatizo hilo na hasa kama linahusiana na upungufu wa umeme nchini na ni kwanini lilionekana kuathiri sehemu kubwa ya nchi.

DA'JESSY: MIFUPA HII INA SIRI

Na. Jessica L Fundi

Habari za kugundulikwa kwa mafuvu yapatayo 40 huko Shinyanga zina-paswa kumshtua kila Mtanzania. Ni habari ambazo zina-paswa kuufanya mwili uteteme lakini pia zinaibua maswali lukuki.



Ni mabaki ya kina nani haya? Jibu hili litasaidia kupata majibu ya jinsi gani walikufa/uawa na kina nani waanahusika.

Kama maelezo ya Mkuu wa Polisi Kamanda Shaibu Ibrahim kuwa mifupa hiyo inaonekana ni ya zamani basi udadisi zaidi unahitajika na hasa uchunguzi wa kisayansi. Kabla haijafikia mahali pa kudai ushirikina au

vitu kama hivyo ni vizuri timu nzuri ya kisayansi ifanye uchunguzi hasa kutokana na kukutwa kwa mifupa hiyo mahali pamoja kitu ambacho kinaashiria vitendo vya makusudi kuiweka hapo.

Ni nani atakuwa na maslahi ya kuiweka miili hiyo hapo? Kwa wanaokumbuka historia yetu kumekuwapo na mauaji ya vikongwe na watu wanaotuhumiwa uchawi huko Shinyanga kwa muda mrefu. Lakini uwezekano kuwa watu karibu 40 waweza kuwa waliuawa bila vyombo vyetu vya usalama kugundua unatisha.

Lakini la kutisha zaidi ni yale yanayoendelea sasa maeneo mbalimbali ambapo Watanania Maalibino wamekuwa wakiuawa katika mazingira ya kishirikina.

Tunaamini kuwa serikali itakuwa tayari na kwa haraka kuliambia Taifa kile kilichogun-



duliwa huko Shinyanga. Kama ni sehemu ya mambo ya Kale (kabla ya kuwa hata Taifa) na hata

kama ni ya hivi karibuni tunaamini kuwa mifupa hii ina historia na siri ambayo inataka kufunua. Ni siri ambayo ilifichikana kwa muda mrefu na sasa imeanza kufunuka.

Vifo vya watu hawa ni lazima vipatiwe maelezo ya kisayansi na kama ipo haja ya kufanyia mazishi rasmi basi hilo nalo lifanyike. Vyovyote vile ilivyo tusikie mifupa hii ina kisa gani cha kutueleza.

Email: dajessy@klhnews.com

MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

Picha za Wiki



Naeem Gire mshirika wa "kampuni" ya Richmond alipofikishwa Kisutu wiki iliyopita.

PATA HABARI MOTOMOTO NA MIJADALA

<http://www.mwanakijiji.com>

Jiandikishe kushiriki mijadala, kupata habari, kusikiliza muziki masaa 24 na matanzazo ya moja kwa moja kila mwishoni mwa juma.

Ukizungumzia habari, unatuzungumzia

KATUNI ZA WIKI



KUTOKA KWENYE MTANDAO

Ushindi wa Obama una maana kubwa kwa sio tu Afrika bali kwa dunia, likija suala la ubaguzi wa rangi. Mtu anatakiwa aheshimiwe mawazo yako bila kujali rangi yake. Na hili ni fundisho kwetu waTZ, uchaguzi wa mwaka 2005 suala la rangi liliingia vibaya mno. Kumbuka Salim alivyokuwa anitwa Mwarabu, lakini haikuangaliwa historia yake ya nyuma jinsi alivyolitumikia Taifa mpaka kuwa Katibu Mkuu wa OAU sasa AU.—**Mfumwa**

Hivi, ni nani kati yenu, anayeweza kuruhusu rafiki yake wa karibu akamatwe, hata kama amekosea?, na ni Kiongozi gani katika awamu zote tatu zilizopita aliyeweza kuwa jasiri akaruhusu marafiki na viongozi wenzake wakamatwe na kufikishwa katika vyombo vya dola kama si Rais Kikwete—**Dr. Harrison Mwakymbembe**

Ulitegemea Mwakymbembe aseme nini? Yeye na JK lao moja tangu walipokuwa mawaziri. Hakuna jipya hapo, kizazi kilichopotea. Pamoja na hilo, mkono mtupu haulambwi. Hivi ni chama gani

cha upinzani ambacho kingemtaka/kumwomba Mwakymbembe ajiunge nacho? - **Dua**

Visingizio vya kushindwa au kutofanya jambo lolote kwa mtu mwenye mawazo ya kimasikini siku zote huwa ni ukosefu wa mtaji, ukosefu wa fedha au ukosefu wa fungu, vyovyote vile ili mradi kisingizio kilenge fedha. Fedha halijawahi kuwa tatizo, tatizo kubwa kwa masikini wote duniani ni ukosefu wa ubunifu, mipango na utekelezaji wa mipango.—**Madela wa Madilu**

Ina maana muda wote tangu ATCL ipate tatizo hakuwahi kukaa na hao jamaa wampe majibu ya hayo maswali? Ana priorities zipi kama hili halikuwa mojawapo? Hivi jamaa amesoma Uchumi kweli? - **John Shaaban**

Kwa hiyo hata ukibadilisha bodi (ya ATCL) na uongeze mtaji bila ya kubadilisha utawala utakuwa unatwanga maji kwenye kinu! - **Bulesi**

TOA NAKALA MOJA

Cheche za Fikra
Mchapishaji na Mhariri Mtendaji

M. M. Mwanakijiji

Timu ya Waandishi
Benjamin Mwalukasa— Mhariri

Freddy Katunzi— Habari za Siasa

Mahmoud Rashid— Habari mbalimbali

Jessica L. Fundi— Makala

Kwa kujiandikisha,
maoni, habari, na ushauri

Tuandikie:
mhariri@klhnews.com

Tovuti: **<http://www.mwanakijiji.com>**

Kanusho: Mawazo yanayonukuliwa hayawakilishi msimamo au mawazo ya mchapishaji na utawala wa kijarida hiki.